

TANGAZO LA SERIKALI NA. 33 la tarehe 24/02/2017

(SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA, (MAMLAKA ZA MIJI)
(SURA YA 288)

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya kifungu cha 89

SHERIA NDOGO ZA (HIFADHI YA BARABARA) ZA HALMASHAURI YA MJI WA
MAFINGA, 2017

- | | | |
|----------------------------|----|---|
| Jina na mwanzo wa kutumika | 1. | Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Kuzuia Uharibifu wa barabara) Halmashauri ya Mji wa Mafinga, 2017 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. |
| Matumizi | 2. | Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la mamlaka ya Mji wa Mafinga. |
| Tafsiri | 3. | Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelekezwa vinginevyo:
“Afisa muidhiniwa” maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.
“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Mji wa Mafinga.
“Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri au Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.
“Watumia barabara” maana yake ni madereva wa magari, pikipiki, baiskel, guta, bajaji, powertiller, na watembea kwa miguu. |

Sheria Ndogo za (Kuzuia Uharibifu wa Barabara)

Tangazop la Serikali Na. 33 (linaemdelea)

- Matumizi sahihi ya barabara
4. Matumizi sahihi ya barabara ni pamoja na;
- (a) Uwezo wa barabara kupitisha magari yenye uzito kama itakavyokuwa imeelekezwa.
 - (b) Watumia barabara mbalimbali lazima wazingatie na kufuata alama za barabarani
 - (c) Watumia barabara wote lazima wazingatie usafi wa mazingira kwa kutotupa takataka ovyo.
- Ukaguzi
5. Kutakuwa na ukaguzi wa uzito wa magari ambapo;
- (1) Maafisa watendaji wa vijiji/mitaa, kata na Afisa mwingine yeyote atakayekuwa ameidhinishwa na Halmashauri atakagua uzito wa magari yanayopita katika maeneo yao.
 - (2) Magari au vizuizi vilivyowekwa na Halmashauri vitakuwa ni vituo vya kukagua uzito wa magari.
- Ukubwa wa barabara
6. Ukubwa wa eneo la barabara itakuwa ni kama ifuatavyo:
- (a) Barabara za kitaifa na mikoa ni mita tisa (9m) (Trunk Roads)
 - (b) Barabara zinazounganisha Wilaya na Mikoa ni mita nane (8m) (collector Roads)
 - (c) Barabara za Halmashauri ambazo zinaunganisha vijiji, kata na Wilaya ni mita saba (7.0m) (Feeder Roads)
 - (d) Barabara za jumuiya ambazo zinaunganisha mtaa na mtaa au kitongoji na kitongoji pamoja na kijiji ni mita saba (7m) (community Roads)
- Upana wa Barabara
7. Upana wa barabara mbalimbali pamoja na hifadhi yake utakuwa;
- (a) Barabara kuu na za mikoa ni mita sitini, upana kutoka katikati ya barabara ni mita thelathini kwa kila upande.
 - (b) Barabara zinazounganisha Wilaya na Mikoa ni mita ishirini kwa kila upande
 - (c) Barabara za Halmashauri zinazounganisha vijiji, kata

Sheria Ndogo za (Kuzuia Uharibifu wa Barabara)

Tangazop la Serikali Na. 33 (linaemdelea)

- na Wilaya ni mita thelathini , upana kutoka katikati ya Barabara ni mita kumi na tano kwa kila upande.
- (d) Barabara za jumuiya ambazo zinaunganisha mtaa na mtaa au kitongoji na kitongoji pamoja na kijiji ni mita ishirini, upana kutoka katikati ya Barabara ni mita kumi kwa kila upande.
- Makosa 8 Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi ikiwa;
- (a) Atapita na gari lenye uzito unaozidi tani kumi kwenye barabara za Halmashauri
 - (b) Atafanya shughuli yoyote ya kibinadamu pembeni ya barabara kama vile kujenga, kulima, kukata miti na kufyatua tofali katika eneo la hifadhi ya barabara.
 - (c) Ataangushia miti barabarani, kuweka magogo na kuacha majani barabarani.
 - (d) Ataacha gari bovu barabarani bila alama za tahadhari.
- Adhabu 9 Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na Masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyoziidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungo.
- Kufifisha kosa 10 Mkurugenzi wa Halmashauri anaweza kufifilisha kosa kwa kumtoza faini ya shilingi elfu hamsini (50,000/=) mtu yeyote chini ya Sheria Ndogo hizi iwapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi na kukubali kulipa faini anayodaiwa kwa kujaza fomu maalumu iliyoandaliwa na kama inavyoonyeshwa kwenye Jedwali la Sheria Ndogo hizi.

Sheria Ndogo za (Kuzuia Uharibifu wa Barabara)

Tangazop la Serikali Na. 33 (linaemdelea)

—
JEDWALI
—

HATI KUFIFILISHA KOSA

(Limetungwa Chini ya kifungu cha 10)

Mimi.....nakiri mbele
ya.....Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Mafinga
kwamba mnamo tareheya mwezimwaka.....nilitenda/nimetenda
kosa la kukiuka masharti ya kifungu chacha Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Barabara)
za Halmashauri ya Mji wa Mafinga za mwaka, 2017.

Nipo tayari kulipa faini ikiwa Mkurugenzi ataamua kutekeleza mamlaka aliyopewa chini ya
Sheria Ndogo hizi.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni kweli nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu
wangu.

Tarehe.....

Saini.....

SAADA S, MWARUKA,
Mkurugenzi
Halmashauri ya Mji wa Mafinga

CHARLES JOHN MAKOGA,
Mwenyekiti
Halmashauri ya Mji wa Mafinga

NAKUBALI,

Dodoma,
9 Januari, 2017

GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB.)
Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI